Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Ya Husaini Bin Ali

Kwa jina lako Jalali nasema yenye ukweli
Ya Husaini Bin Ali niwe nikihadithia

Mama yake ni Fatima, na babu yake Hashima
Na Madina mji mwema, ndiko alikozaliwa

Na Sayidina Husain, kaka yake ni Hasan
Akiwapenda amini, kisha akiwa sifia

Mtume amebaini, ya kama huyu Husaini
Na mwingine ni Hasani, Peponi wataingia

Yaani wao ni mabwana, wa peponi vijana
Subhana maulana, wote amewaridhia

Ni mwezi wa Shaabani, alozaliwa Husain
Na siku yake yakini, ni jumanne sikia

Mwaka wa nne Hijira, ndio kazawa mbora
Na siku ya saba mara, kamwakikiya Nabia

Mtume kamwadhinia, sikioni la kulia
Kinywa kamsugulia, kwa mate halafu nia

Alikuwa ni mzuri, wa umbo la kunawiri
Sura kama ya bashiri, kwani kamshabihia

Akipigania dini, kwa udhati moyoni
Hajali nini na nini, ila dini ya jalia

Husaini akiwa Maka, aliupata waraka
Kuwa aende haraka, Iraqi kum-baiya

Watu wangu simameni, twende Iraqi mjini
Aliwambia Husaini, nao wakafuatia

Husaini aliambiwa, huko acha kuendea
Twakusihi kusikia, huko hapatakufaa

Abdallah wa Abasi, Kasema kinga nafsi
Zao japo wafuasi, japo na watoto pia

Wende wewe peke yako, sio na ahali zako
Bwana kwa hisani yako, shika ninayokwambia

Bwana Husaini kasema, Kwenda huko ni lazima
Litalonipata ni jema, Mimi nimesafi nia

Nikenda wakiniuwa, peponi nitaingia
Kwani nimesafi nia, dini kuisimamia

Liwalo lote na liwe, Iraqi ni paendewe
Sio mimi nihofie niache kupaendea

Hapo Seyyidi Husaini, Katoka Makka mjini
Na watu wake sabini, Wote wakamfatia

Wenye farasi yakini, walikuwa thalathini
Wengine arubaini, kwa miguu ilikuwa

Alipokuwa njiani, wakazidi yakini
Mia moja khamsini, ndio waliozidiya

Hao mia khamsini, walirudia njiani
Hawakumfata Husain, hadi Iraqi sikiya

Husaini na watu wake, ni Iraqi Wapafike
Na taabu iwafike, kwa humo Karbala

Mto ulio karibu, nae Husaini Muhubi
Alizuiwa ajabu, na maadui kutumia

Maji wakazuiliwa, wasiwe wayatumia
Kambi akajipigia, bwana Husaini sikia

Akawa maji anyimwa, huku kiu chawauma
Watoto wanalalama, kwa vile wanaumia

Husaini na watu wake, ati wao wateseka
Na maji yasitumike, kunywewa na watu hawa

Hapo Husaini hakika, vikali aliteseka
Watoto walalamika, Baba! Baba! twaumia

Jeshi hilo lilikuwa, kabisa lamzuia
Husseini kukaribia, maji yale kutumia

Watoto waliumia, kwa kiu kuwazidia
Kati yao alikuwa, mtoto mdogo pia

Mtoto huyu ni Ali, alizidiwa kikweli
Zeinabu binti Ali, sana sana alilia

Machozi yalimtoka, mengi yakatiririka
Akayafonza hakika, mtoto kujimezeya

Zeinabu binti Ali, ni shangazi lake Ali
Kwa ala kulihali, machozi maji yakawa
Hata ile siku ya Ashura, kwa mwezi kumi dhahira
Muharamu ndio mara, wakaanza kuuwawa

Kwanza wafuasi wake, kisha wa nyumbani kwake
Alibaki ye na chake, kijitoto kikilia

Umri miezi sita, hivyo hanavyo matata
Hivyo maji angepata, yangali msaidia

Mtoto mchanga yule, wakampiga mishale
Na mtoto pale pale, aliiaga dunia

Kisha wakamzunguka, Husaini mwenye baraka
Wakamuuwa hakika, nae kaaga dunia

Baada ya kumuuwa, hema moto walitia
Hata wakawachukua, banati zake Nabiya

Wakawafanya mateka, kisha wakawapeleka
Huko Kufa kupafika, bila kuwahurumia

Ni kwa Ibni Ziyadi, ndiko iliko wabidi
Gavana wake Yazidi, yeye ndie alikiuwa

Hivyo watu wa Iraqi, walikataa haki
Kumuuwa mwenye haki, kipenzi chake Nabia

Kuuwawa kwa Husaini, Ni jambo lenye huzuni
Katu haiwezekani, machozi kuyazuia

Machozi shuti kutoka, na watu kuhuzunika
Kwa kipenzi msifika, kinyume alofanyiwa

Ewe Seyyidi Husaini, ulotoka duniani
Kwa kupigania dini, peponi wenda ingia

Umekufa ni shahidi, hivyo ni kama zawadi
Allahu Mola wadudi, shahidi kakwandikia

Waswalatu wa Salamu, zimfikie Hashimu
Na Husaini Muadhamu, na walio bakiya

Na: Saidi Musa
Zanzibar

Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi Asema:

Imam Hasan na Imam Husain (a.s.) wameuhurisha
Uislamu kutokana na utumwa wa Wafalme na hivyo basi,
Wameuhifadhi kutokana na uharibifu daima.

Wafalme watakuja, na Wafalme watakwenda,
lakini Uislamu utadumu milele.
Kwa Uislamu, majina matakatifu
ya Hasan na Husain yataangaza milele.

Source URL: https://www.al-islam.org/ar/node/40655#comment-0